

Ndugu waheshimiwa, wapendwa wanafunzi na marafiki zetu,

Baada ya wingi wa salamu ni furaha yetu kubwa kutangaza kikao kifuatacho cha

**Baraza letu la Kiswahili la Berlin (BALAKI-BE) la tarehe 8 Novemba 2021**

**Balaa na Beluwa ya Miradi ya Miundombinu ya Uchina (SGR) kwa Wakazi wa Pwani ya Kenya na haswa Jiji la Mombasa**

### **Kadara Swaleh**

Katika wasilisho langu nitazungumzia athari za miradi ya miundombinu ya Uchina kama vile Reli ya Kisasa (SGR) kwa wakazi wa Mombasa na haswa namna ambavyo miradi hii imechafua ajira na kusambaratisha riziki za watu mbalimbali katika jamii. Mbali na Mombasa, nitaangazia pia bandari mpya ya Lamu na maafa yake kwa wakazi wa huko. Ni muhimu kukumbuka kwamba mwaka 2018 serikali ya Kenya ilitoa fatwa ya kwamba shehena zote zinazofika bandari ya Mombasa zisafirishwe kuelekea Nairobi, Naivasha na kwengineko kwa njia ya SGR pekee. Kadhalika, serikali iliamuru kazi ya utendaji ya bandari ihamishwe Mombasa na ipelekwe Naivasha ambapo serikali imejenga 'bandari kavu'. Hatua hizi zimewadhaliisha watu wa Mombasa ambao wamekuwa wakitegemea kazi na biashara ya bandari kwa miaka na mikaka. Vilevile, nitaangazia mbinu mbalimbali ambazo watu wa Mombasa wametumia kuhimili maafa na majanga yaliyowapata. Mwisho, nitachambua ni vipi kitu kizuri kama miundombinu hubadilika na kuwa balaa badala ya manufaa.

**Kadara Swaleh** ni mtafiti kwenye taasisi ya ZMO, Berlin, kwenye kitengo cha utafiti kinachoitwa "De:link//Re:link" kinachoangazia mbinu mpya na mitazamo ya ndani ya kufahamu miradi ya miundombinu ya mipaka kama vile miradi ya Ukanda na Barabara (BRI) ya Uchina. Yeye ni mwanafunzi wa uzamili kwenye Chuo Kikuu Huru cha Berlin kwenye Taasisi ya Anthropolojia. Amewahi kusomesha Chuo Kikuu cha Pwani huko Kenya kwa muda mfupi kabla ya kwenda kufanya kazi kwenye taasisi za serikali na uongozi wa vyama vya kisiasa.

Kikao kitafanyika **saa kumi kamili za huku** (saa kumi na mbili kamili za Afrika Mashariki) **hadi saa kumi na mbili kasoro** (saa mbili kasoro za Afrika Mashariki) **kwa njia ya Zoom:**

Muda: 8 Nov 2021 04:00 PM Berlin / 06:00 PM Dar es Salaam & Nairobi

<<https://us02web.zoom.us/j/81451695325?pwd=aUYwanduQ01PdDjhTDNlL25sZjBtQT09>>

ID ya kikao: 814 5169 5325; Code: 966414

**KARIBUNI SANA!**

**Tafadhali wajulisheni wapenzi wote wa Kiswahili na wenzenu wengine!**

Wasalaam,

Kai Kresse, Luti Diegner & Maxwell Omondi

*Mkiva na maswali kubusu baraza hili tafadhalini mwandikieni mwenzetu: <MaxwellOmondi.Ondieki@zmo.de>*